NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

9 Novemba 2018

Kwa Wabaha'i wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Wakati mchakato wa uchangukaji wa utaratibu wa ulimwengu uombolezao wenye mapungufu upatavyo msukumo katika sehemu zote za ulimwengu, ukisababisha utovu wa matumaini, kiwewe, uhasama, na mashaka, mioyo ya marafiki kila mahali lazima ihakikishiwe, macho yao yakiona vyema, miguu yao thabiti, kadiri wafanyavyo kazi kwa subira na kwa kujitoa dhabihu kuinua utaratibu mpya badala yake. Muongozo wa Bahá'u'lláh ni msingi ambao juu yake mnajenga. Maagizo Yake yapo dhahiri: "Mtumishi huyu huisihi kila roho yenye bidii na jasiri kufanya juhudi ya hali ya juu kabisa na kuinuka kurekebisha upya hali katika maeneo yote na kuwahuisha wafu kwa maji ya uzima ya hekima na matamshi, kwa ajili ya upendo authaminio sana wa Mungu, Mmoja, Asiye kifani, Mwenye enzi, Mpaji." Tiba Yake takatifu imeagizwa: "Mungu, Mkweli, hunishuhudia Mimi, na kila chembe iishiyo imesukumwa kuthibitisha kwamba njia kama hizo kama ziongozavyo kwenye uinuaji, maendeleo, elimu, ulinzi na wongofu wa watu wa dunia zimewekwa dhahiri Nasi na zimefunuliwa na Kalamu ya Utukufu katika Vitabu Vitakatifu na Nyaraka." Na uhakikisho Wake umepachikwa juu ya kila moyo mwaminifu: "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kupitia matendo safi na mema, kupitia mwenendo usifikao na unaostahili."

Wakati wa utumishi wa 'Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi, jumuiya ya kwanza ya ukubwa wa kutosheleza ambayo ingeweza kuanza kutumia mafundisho ya Bahá'u'lláh kimpangilio ili kuunganisha maendeleo ya kimwili na ya kiroho ilikuwa ile ya waumini waliokuwa katika Chimbuko la Imani. Utiririkaji thabiti wa miongozo kutoka Nchi Takatifu uliwawezesha Wabahá'í wa Iran kupiga hatua kubwa mno katika kipindi cha kizazi kimoja au viwili tu na kuchangia sehemu ya kipekee kwenye maendeleo ya taifa lao. Mtandao wa shule ambao ulitoa elimu ya kimaadili na kitaaluma, ukiwa ni pamoja na kwa wasichana, ulishamiri. Ujinga takribani ulifutwa katika jumuiya ya Kibahá'í. Shughuli za hisani zilianzishwa. Hisia za upendeleo/chuki bila sababu miongoni mwa vikundi vya kikabila na kidini, zilizowaka katika jamii pana, zilizimwa ndani ya upendo ukumbatiao wa jumuiya. Vijiji vikatofautishwa kwa usafi wao, utaratibu, na maendeleo. Na waumini kutoka nchi hiyo walikuwa chombo katika kuinua katika nchi nyingine Mashriqu'l-Adhkár ya kwanza ikiwa na mikondo iliyosanifiwa "kukidhi kitulizo kwa atesekaye, riziki kwa fukara, hifadhi kwa msafiri, faraja kwa mkiwa, na elimu kwa mjinga." Muda ulivyokwenda, jitihada kama hizo zilizidishwa kwa shughuli zilizosambaa za jumuiya za Kibahá'í katika sehemu mbali mbali za ulimwengu. Walakini, kama Shoghi Effendi alivyoelezea kwa jumuiya mojawapo, idadi ya waumini ilikuwa bado ndogo mno kuathiri mabadiliko ya kutambulika katika jamii pana zaidi, na kwa zaidi ya nusu ya karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi waumini walihamasishwa

kuelekeza nguvu zao kwenye utangazaji wa Imani, kwani hii ilikuwa ndiyo kazi ambayo Wabahá'í pekee wangefanya—kwa hakika wajibu wao wa kimsingi wa kiroho—na ingewaandaa kwa ajili ya wakati ambapo wangeweza kushughulikia matatizo ya jamii ya binadamu moja kwa moja zaidi.

Miaka thelathini na tano iliyopita, mazingira ndani na nje ya jumuiya yaliunganika kutengeneza uwezekano mpya kwa ajili ya ujihusishaji mkubwa zaidi katika maisha ya jamii. Imani ilikuwa imefikia kiwango ambapo michakato ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ilihitajika kuingizwa katika shughuli zao za kawaida, na Oktoba 1983 tuliwaomba Wabahá'í wa ulimwengu kuingia katika uga huu mpya wa jitihada. Ofisi ya Miradi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi ilianzishwa kwenye Makao Makuu ya Ulimwengu ya Imani ili kutusaidia kuendeleza na kuratibu shughuli za marafiki kote ulimwenguni. Shughuli za Kibahá'í kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kwenye kiwango chochote kile cha utata, wakati huo zilihesabika katika mamia. Leo zinafikia makumi ya maelfu, ikiwemo mamia ya miradi endelevu kama vile shule na korija za mashirika ya maendeleo. Mlolongo mpana wa shughuli za sasa huvuka jitihada kutoka vijiji na ujirani hadi mikoa na mataifa, zikishughulikia msululu wa changamoto, ikiwemo elimu kutoka awali hadi chuo kikuu, kusoma na kuandika, afya, mazingira, misaada kwa wakimbizi, maendeleo ya wanawake, uwezeshaji wa vijana chipukizi, ukomeshaji wa hisia za upendeleo/chuki ya mbari, kilimo, uchumi wa maeneo, na maendeleo ya vijiji. Nguvu ya Hoja ya Bahá'u'lláh ya ujenzi wa jamii imeanza kuonekana kuwa yenye mpangilio zaidi katika maisha ya pamoja ya marafiki kama matokeo ya uchapuzaji wa mchakato wa upanuzi na uimarishaji, hususani katika klasta zilizopiga hatua. Mbali na hili, bila shaka, waumini wasiohesabika, kupitia jitihada za kitaalamu na za kujitolea, huchangia nguvu na umaizi wao kwa miradi na mashirika yaliyoanzishwa kwa ajili ya maslahi ya wote.

Kwa mara nyingine tena, tunaona kwamba nguvu zilizoko ndani na nje ya Imani zimefanya uwezekano wa hatua mpya katika kazi ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika ulimwengu wa Kibahá'í. Kwa hiyo, kwenye tukio hili takatifu la Sherehe Pacha za Kuzaliwa, tuna furaha kutangaza kwamba Ofisi ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwenye makao makuu, sasa imechanua katika asasi mpya ikumbatiayo ulimwengu iliyoanzishwa kwenye Makao Makuu, Shirika la Kibaha'i la Maendeleo la Kimataifa. Aidha, Mfuko wa Maendeleo wa Kibahá'í, utazinduliwa, ambamo shirika jipya litachota fedha kusaidia jitihada zote mbili; zile zilizokuwepo kwa muda mrefu na zile zinazoibuka za maendeleo kote ulimwenguni; utasaidiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, na watu binafsi na asasi zinaweza kuuchangia.

Bodi ya wakurugenzi yenye wajumbe watano itateuliwa ambayo itafanya kazi kama shirika la kiushauriano ili kuendeleza na kuratibu jitihada za jumuiya kote ulimwenguni katika miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Wakurugenzi watahudumu kwa muhula wa miaka mitano kuanzia Siku ya Agano. Ikitenda kazi kwenye kituo cha kiroho na kiutawala cha Imani, bodi itashauriana na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa ili kuhakikisha kwamba kazi ya maendeleo inapatana na jitihada nyingi za ulimwengu wa Kibahá'í. Asasi hii mpya itaanza kwa kuendeleza kazi na mamlaka yaliyokuwa yakitekelezwa hapo awali na Ofisi ya miradi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi na kisha pole pole kukua katika uwezo kuyatekeleza katika kiwango kipanukacho na kwenye viwango vya juu zaidi vya utata. Itaendeleza jitihada za Wabahá'í mmoja mmoja, jumuiya, na asasi kote ulimwenguni ili kupanua na

kuimarisha kiwango cha shughuli zao. Itasaidia kuimarisha uwezo wa kiasasi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jumuiya za kitaifa, ikiwemo kupitia uundwaji wa mawakala wapya na uibukaji wa mashirika ya maendeleo. Itakuza katika kiwango cha kimataifa, mbinu za maendeleo na njia ambazo zimethibitisha kufaa. Itajiweka karibu na matokeo ya mambo yanayotokea katika uga wa maendeleo na kuchunguza matumizi yao patanifu na kanuni za kiroho kwa msaada kutoka kwa Wabahá'í walio na mafunzo stahiki. Itaunda mitandao ya nguvu kazi na mipangilio ya kiasasi katika mabara yote kadiri ihitajikavyo kwa ajili ya utekelezaji wa njia zake mbali mbali za kiutendaji. Juu ya yote, kama ilivyokuwa Ofisi ya Miradi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi kabla yake, kusudi lake la kimsingi litakuwa kusimamia ujifunzaji kuhusu maendeleo kwa kukuza na kusaidia utendaji, tafakari juu ya utendaji, kujifunza, kushauriana, kukusanya na upangiliaji wa tajiriba, ubunifu, na mafunzo—yote yakitekelezwa kwa kuzingatia Mafundisho ya Imani.

Kwenye Tao juu ya Mlima Carmel ambalo huzunguka sehemu za mapumziko ya wana-Familia Takatifu, Shoghi Effendi alitarajia vyote viwili uinuliwaji wa majengo na uanzishwaji wa asasi za kimataifa—kiutawala, kisayansi, na kijamii—ambayo yangeshamiri chini ya kivuli cha Imani ya Bahá'u'lláh. Asasi hii mpya kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi itakua na kubadilika kwa miongo na karne za usoni kulingana na mahitaji ya jamii ya binadamu na chini ya maelekezo ya Nyumba ya Haki hadi ustaarabu wa kimwili na kiroho uliotarajiwa na Bahá'u'lláh utakapofikiwa katika ulimwengu huu wa nasibu.

Hatimaye, bila shaka, kazi ya miradi ya Kibahá'í ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi imo mikononi mwa marafiki kila mahali. Ili kutumia fursa kamili zinazoibuka, mtu asingehitaji kuangalia zaidi kwenye hamasa na umaizi bali kwenye Mfano Kamili wa mafundisho ya Kibahá'í. Fikiria maneno Yake: "Tunapaswa tuendelee daima kuanzisha misingi mipya kwa ajili ya furaha ya wanadamu na kubuni na kuendeleza njia za kulitimiza hili. Ni bora jinsi gani, ni heshima jinsi gani kama mtu akiinuka kutimiza majukumu yake; inapotosha na kudharaulika jinsi gani, kama akifumba macho yake kwa ustawi wa jamii na kupoteza maisha yake ya thamani katika kushughulikia maslahi yake ya kibinafsi na manufaa binafsi. Furaha kuu ni ni ya mtu, na anashuhudia ishara za Mungu katika ulimwengu na katika roho ya binadamu, kama akipanda farasi bora wa jitihada ya hali ya juu katika uwanja wa ustaarabu na haki."

Nyumba Ya Haki Ya Ulimwengu